**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA UCHUKUZI**

**MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI**

LATRA
IMETHIBITISHWA ISO 9001

# TAARIFA KWA WANAHABARI

## MAFANIKO YA LATRA KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MITANO YA UONGOZI WA MHE. DKT SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA (AWAMU YA SITA)

*Dar es Salaam, 24 Septemba 2026*

### 1.0 UTANGULIZI

**Ndugu Wanahabari,** Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia uzima, na fursa ya kukutana nanyi tena kwa lengo la kuendelea kutoa taarifa kuhusu mafanikio ya utendaji wa LATRA katika kipindi cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya **Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**. Leo tutawajuza kwa uchache mafanikio ya LATRA katika kipindi cha miaka mitano (5), 2021/22 hadi 2025/26.

**Pili,** napenda kutumia fursa hii kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti, na wafanyakazi wa LATRA, kuendelea kutoa Pongezi za dhati na za moyoni kwa **Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, kwa Uongozi wake mahiri unaokuza shughuli za kijamii na kiuchumi Nchini, wenye mafanikio mengi makubwa, ulioweka mazingira mazuri ya uwekezaji katika sekta ya uchukuzi, na kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa urahisi chini ya falsafa yake ya **4-R (Reconciliation – Maridhiano, Resilience – Ustahimilivu, Reforms – Mageuzi, na Rebuilding – Kujenga upya).** LATRA tumekuwa tukizingatia sana fasalfa ya 4-R, na kwa hakika **Uongozi wa Mhe. Rais, Dkt Samia Suluhu Hassan umetujengea mazingira rafiki sana ya ushirikishaji wa wadau wetu katika sekta ya uchukuzi na hivyo kuleta maelewano bila migongano**. Tunawapongeza pia wasaidizi wake wanaotusimamia, wakiwemo **Mhe. Prof. Makame Mbarawa (Mb), Waziri wa Uchukuzi, Mhe. David Kihenzile (Mb), Naibu Waziri wa Uchukuzi, Prof. Godius W. Kahyarara, Katibu Mkuu, Wizara ya Uchukuzi,** na **Bw. Abdallah Mitawi, Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Uchukuzi.**

**Tatu,** napenda kutumia fursa hii kuendelea kuwashukuru sana **watoa huduma** zinazodhibitiwa na LATRA, **watumiaji wa huduma** za usafiri ardhini, Baraza la watumiaji wa huduma za LATRA (LATRA CCC) pamoja na **wadau wote wa usafiri ardhini**, ikiwa ni pamoja na taasisi za umma na sekta binafsi kwa ushirikiano waliotupatia katika katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yetu. LATRA inatambua na kuthamini sana ushirikiano mkubwa kutoka kwa kila mdau na kupitia vyama vyao ikijumuisha wasafirishaji wa abiria (wakiwemo TABOA, AKIBOA, DARCOBOA, UWADAR, MABOA, MTA), wasafirishaji wa mizigo (wakiwemo TAT, TATOA, TAMSTOA, na TRFA), na watoa huduma za usafiri wa kukodi na mawakala wetu (wakiwemo LGAs, Shirika la Posta Tanzania, MAUPIDA SACCOS Ltd, BAPIMMO SACCOS Ltd, KIBABOT SACCOS Ltd, UWAMWA SACCOS Ltd, Bolt, Balagum Investment Company Limited, Bachoji, Auction Mart Ltd ,Tambaza Auction Mart, Daladala Logistics), Madereva na makondakta (TADWU) LATRA itaendelea kuuenzi ushirikiano uliopo katika kutekeleza majukumu yetu kwa weledi, na kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu zilizopo

**Nne,** tunaendelea kuwashukuru sana ninyi **Wanahabari pamoja na Wamiliki wa Vituo na Vyombo vya Habari** kwa kutumia vyema taaluma zenu katika kuuhabarisha na kuuelimisha umma. **Wino wa Kalamu zenu una thamani kubwa sana katika kujenga Taifa** lenye watoa huduma za usafiri wanaozingatia misingi ya Sheria kutoa huduma bora na Taifa lenye watumia huduma za usafiri wanaotambua haki na wajibu wao na njia sahihi za kudai haki zao kwa mujibu wa Sheria. Aidha **kalamu zenu zinathamani kubwa katika kujenga Taifa lenye umoja, upendo, mshikamano, maelewano, utulivu na amani.** Asanteni sana, **tutaendelea kuwathamini na kuthamini kazi zenu**.

**Mwisho**, sio kwa umuhimu, nitumie fursa hii kumshukuru **Bw. Nehemia Mchechu, Msajili wa Hazina na Menejimenti yake** kwa usimamizi wao wa Taasisi na Mashirika ya Umma, lakini Zaidi, kwa kuendelea kuratibu utaritibu huu wa kukutana nanyi na kuuhabarisha umma kuhusu utendaji na mafanikio ya Taasisi na Mashirika ya Umma.

## 2.0 KUANZISHWA KWA LATRA, MAJUKUMU NA WAJIBU WAKE

**Ndugu Wanahabari,** napenda kuwajulisha kwa ufupi kuanzishwa kwa LATRA, Ofis iza LATRA Nchini, pamoja na majukumu na wajibu wa LATRA kama ifuatavyo:

### 2.1 Kuanzishwa kwa LATRA

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ilianzishwa kwa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini Sura 413 ili kudhibiti huduma za usafiri kwa njia ya Reli, Barabara na Waya; ikipokea majukumu haya kutoka Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA). LATRA ilianza kazi rasmi mnamo tarehe 29 Aprili, 2019 baada ya Sheria yake kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Namba 358 la tarehe 26 Aprili, 2019.

### 2.2 Ofisi za LATRA

LATRA ina **ofisi katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara**. Aidha, katika kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya Sita, LATRA imeendelea kusogeza huduma zake karibu na wananchi kwa kufungua **ofisi kumi na nne (14)** katika maeneo ya kimkakati kwenye baadhi ya miji na wilaya nchini. Maeneo hayo ni Kituo cha Mabasi cha **Magufuli - Mbezi, Tegeta, Mbagala, na Kituo cha Ufuatliajai wa Magari (VTC) kilichopo Mikocheni (Dar es Salaam).** Maeneo mengine ni **Makambako (Njombe), Kahama (Shinyanga), Masasi (Mtwara), Ifakara (Morogoro), Korogwe (Tanga), Same (Kilimanjaro), Nzega (Tabora), Karatu (Arusha), Chunya (Mbeya), na Mkuranga (Pwani).** Haya ni mafanikio makubwa. Aidha, taratibu zinaendelea ili kufungua Ofisi nyiingine saba (7) katika maeneo ya **Gongo la Mboto (Dar es Salaam), Boma Ng'ombe (Kilimanjaro), Tunduru (Songea), Mufindi (Iringa), Kituo cha mabasi Nyegezi na Nyamhongolo Mwanza)** na **Dumila (Morogoro).**

### 2.3 Majukumu na Wajibu wa LATRA

#### (a) Majukumu ya LATRA

Kifungu cha 5(1) cha Sheria ya LATRA, kinaelekeza majukumu yafuatayo:

a) Kutekeleza majukumu yaliyo chini yake kwa mujibu wa Sheria za kisekta (Sheria ya Leseni za Usafirishaji, Sura ya 317, na Sheria ya Reli, Sura ya 170);
b) Kutoa, kuhuisha na kufuta leseni na vibali vya usafirishaji;
c) Kwa kuzingatia Sheria za Kisekta;
   i. kusimamia viwango vya ubora wa huduma na usalama katika sekta;
   ii. kusimamamia viwango na masharti ya utoaji wa huduma zinazodhibitiwa;

iii. kudhibiti viwango vya tozo za huduma zinazodhibitiwa.

d) Kusajili wahudumu na kuthibitisha madereva wa sekta zinazodhibitiwa;

e) Kuthibitisha ubora wa vitembea reli (rolling stock), na miundombinu ya reli (railway infrastructure);

f) Kusimamia utendaji wa sekta zinazodhibitiwa ikijumuisha:

i. viwango vya uwekezaji,

ii. uwepo wa usalama, ubora, na viwango vya huduma,

iii. gharama za huduma,

iv. ufanisi wa uzalishaji (uandaaji) na usambazaji (utoaji) wa huduma, na

v. masuala mengine yanayohusiana na Mamlaka.

g) Kuwezesha utatuzi wa malalamiko na migogoro;

h) Kutoa taarifa ya masuala yanayohusu majukumu ya Mamlaka;

i) kushauriana na mamlaka nyingine za udhibiti au vyombo au taasisi zinazotekeleza majukumu sawa na ya Mamlaka Tanzania Bara au mahali pengine popote; na

j) Kutekeleza majukumu mengine ambayo yamewekwa na Sheria ya LATRA au sheria nyingine za kisekta.

**(b) Wajibu wa LATRA**

Kifungu 6 cha Sheria ya LATRA, Sura ya 413 kinaeleza Wajibu wa LATRA kuwa, katika utendaji wake, itahakikisha inakuza ustawi wa jamii ya Watanzania kwa:

a) kukuza ushindani na ufanisi wa kiuchumi katika kutoa huduma za usafiri ardhini;

b) kuimarisha usalama wa huduma za sekta zinazodhibitiwa ikijumuisha usalama wa watumiaji wa huduma za sekta zinazodhibitiwa;

c) kulinda maslahi ya watumiaji kwenye gharama, ubora, na viwango vya huduma za usafiri ardhini;

d) kulinda uwekezaji wa watoa huduma wenye ufanisi;

e) Kuhakikisha huduma zinapatikana na kufikiwa na watumiaji wote wakiwemo watu wenye vipato vidogo, wakazi wa vijijini na watu wenye mahitaji maalum;

f) kuelimisha umma kuhusu sekta zinazodhibitiwa, kazi na wajibu wa Mamlaka, haki na wajibu wa watumiaji, uwasilishaji wa malalamiko, migogoro na utatuzi wake; na

g) kutunza na kulinda mazingira.

## 3.0 DIRA, DHAMIRA NA MISINGI MIKUU

**Ndugu Wanahabari,** Pamoja na kuongozwa na misingi ya Sheria, LATRA inazingatia **Dira (Vision), Dhamira (Mission) na Misingi Mikuu (Core Values)** iliyojiwekea na kuifuata kwenye utendaji kazi na majukumu ya kila siku.

***a) Dira:*** *Kuwa Nchi yenye huduma za usafiri ardhini zilizo salama, za kuaminika na endelevu.*

***b) Dhamira:*** *Kudhibiti huduma za usafiri ardhini kupitia utoaji wa leseni, ufuatiliaji na uendelezaji wa ushindani wa haki kwa ajili ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya Watanzania.*

***c) Misingi Mikuu:*** LATRA inaongozwa na misingi mikuu ifuatayo:

i) **Utaalamu (Professionalism):** Kutekeleza majukumu kwa weledi, umahiri na kuzingatia viwango vya kitaaluma;

ii) **Uwajibikaji (Accountability):** Kuwajibika kwa matokeo ya maamuzi na utekelezaji wa majukumu yetu;

iii) **Ushirikiano (Teamwork):** Kufanya kazi kwa pamoja kwa kuzingatia mshikamano na kufanikisha malengo ya Taasisi;

iv) **Uadilifu (Integrity):** Kutenda kwa uaminifu, maadili na kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa;

v) **Uwazi (Transparency):** Kutoa taarifa na kutekeleza majukumu yetu kwa uwazi na kwa kuzingatia haki; na

vi) **Ubunifu (Innovativeness):** Kuendeleza na kutumia mawazo, teknolojia na mbinu mpya katika kuboresha huduma na utendaji wa Taasisi.

## 4.0 MAFANIKIO YA LATRA KATIKA MIAKA MITANO, 2021/22 – 2025/26

**Ndugu Wanahabari,** Mafanikio ya LATRA katika kipindi cha miaka mitano (05) ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi wa **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,** kuanzia mwaka wa fecha 2021/22 hadi 2025/26 ni kama ifuatavyo: -

### 4.1 Udhibiti Usafiri wa Barabara

#### 4.1.1 Utoaji Leseni kwa Vyombo vya Usafiri kwa Njia ya Barabara

Kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1)( b) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Sura ya 413, LATRA ina wajibu wa **kutoa, kuhuisha, kusitisha na/au kufuta leseni za usafirishaji**. Idadi ya leseni za usafirishaji zilizotolewa kwa vyombo vya usafiri wa abiria (passenger service vehicles), mizigo (goods carrying vehicles), na vyombo vya usafiri wa kukodi (private hire service vehicles) ziliongezeka kutoka leseni **239,953** mwaka wa fedha **2021/22** hadi leseni **590,468** mwaka wa fedha **2025/26**, ikiwa ni ongezeko la **leseni 350,515,** sawa na ongezeko la jumla la **asilimia 146.1.** Ongezeko hili ni sawa na wastani wa ukuaji wa **asilimia 27.2** kwa mwaka. Muhtasari wa idadi ya leseni zilizotolewa katika kipindi cha miaka mitano (5) kuanzia mwaka wa fedha 2021/22 hadi 2025/26 yanaoneshwa kwenye Jedwali Na 01:

**Jedwali Na. 01: Idadi ya Leseni Zilizotolewa Mwaka 2021/22 – 2025/26**

| Na. | Kundi la Leseni | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Magari ya Abiria (Public Service Vehicle) | 34,967 | 36,958 | 33,380 | 34,688 | 29,654 |
| 2 | Magari ya Mizigo (Goods Carrying Vehicles) | 143,011 | 169,942 | 192,996 | 210,749 | 238,733 |
| 3 | Magari ya Kukodi (Private Hire Vehicles) | 61,975 | 77,258 | 100,200 | 107,754 | 322,081 |
| | **Jumla** | **239,953** | **284,158** | **326,576** | **353,191** | **590,468** |
| | **Ongezeko kwa Mwaka (%)** | | *18.4* | *14.9* | *8.1* | *67.2* |

***Chanzo:*** *LATRA, 2026*

#### 4.1.2 Uthibitishaji wa Madereva na Usajili wa Wahudumu

Kwa mujibu wa Kifungu cha 5(1)(d) cha Sheria ya LATRA Sura 413, LATRA ina jukumu la kusajili wahudumu na kuthibitisha madereva na kusajili wahudumu wa vyombo vya usafirishji vinavyodhibitiwa. Lengo la kuthibitisha madereva na kusajili wahudumu ni kuhakiki weledi wa madereva kuendesha magari yanayotoa

huduma za usafiri wa umma na mizigo kwa usalama, na kuwa na wahudumu wenye kuelewa Sheria, Kanuni na Taratibu ili kuboresha utoaji wa hudumu unaowaridhisha watumiaji. Matokeo ya utekelezaji wa jukumu hili ni kama ifuatavyo:

**a) Kuthibitisha Madereva wa Magari yanayodhibitiwa**

LATRA imeendelea kusajili na kuthibitisha kwa mujibu wa kifungu cha 5(1)(d) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Sura ya 413. Lengo la kwathibitisha madereva ni kufuatilia mienendo yao wakiwa barabarani kupitia mifumo ya TEHAMA (VTS na i-buttons) ili kuboresha weledi na kudhibiti mwenendo wa madereva wakiwa barabarani, hivyo kuleta usalama wa huduma na kuepuka ajali za barabarani. Katika kipindi cha miaka mitatu ya utekelezaji wa jukumu hili (2022/23-2025/26) jumla ya **madereva 15,547** walisajiliwa na **kufanya mtihani wa kuthibitishwa na LATRA** kupitia Mfumo wa Kutahini Madereva (*Drivers Testing System* - DTS) ambapo kati ya hao **madereva 8,642 walifaulu na kuthibitishwa, sawa na wastani wa asilimia 56**. LATRA imeweka utaratibu wa lazima wa madereva wa safari za usiku kwa mabasi ya abiria na mabasi ya kokodishwa kuwa na kitufe cha utambuzi (*i-button*).

Pamoja na kuwa idadi ya madereva wanaofanya mitihani na kufauli imeendelea kukua mwaka hadi mwaka, bado matokeo haya ya ufaulu wa asilimia 56 yanaashiria **maandalizi hafifu kwa madereva, woga wa mitihani unaofanywa kwa kompyuta, upya wa zoezi la kuthibitisha madereva, na kukosekana kwa utaratibu wa kujisomea/kujiendeleza kwa madereva**. Muhtasari wa taarifa za madereva waliofanya mitihani na kufaulu/kuthibitishwa katika kipindi cha 2022/23 hadi 2025/26 yameoneshwa kwenye Jedwali Na 02:

**Jedwali Na. 02: Idadi ya Madereva Waliofanya Mtihani na Kuthibitishwa**

| Na. | Aina ya Vipindi | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Waliofanya Mtihani | 1,707 | 3,879 | 3,605 | 6,356 | **15,547** |
| 2 | Waliofaulu na Kuthibitishwa | 1,061 | 1,952 | 1,550 | 4,079 | **8,642** |
| 3 | Kiwango cha Ufaulu | 62% | 50% | 43% | 64% | **56%** |

***Chanzo:*** *LATRA, 2026*

**b) Kusajili Wahudumu wa Magari yanayodhibitiwa**

LATRA imeendelea na kutekeleza jukumu la kusajili wahudumu wa magari ya abiria kwa mujibu wa kifungu cha 5(1)(d). Hata hivyo, kabla ya wahudumu kusajiliwa, wanapaswa kupata mafunzo maalum kuhusu kazi zao kwenye vyombo vya usafiri ikiwa ni pamoja na kujua Sheria, Kanuni, na Taratibu husika na utoaji wa huduma bora kwa abiria na wateja kwa ujumla. LATRA iliandaa mtaala wa kozi fupi ya wiki moja (masaa 60) kwa kushirikiana na vyuo vya elimu. Mafunzo hayo hutolewa na vyuo vinne (04) ambavyo ni Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Chuo cha Biashara (CBE), Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), na Chuo cha Ufundi Arusha (ATC). Jukumu hili lilianza kutekelezwa mwaka wa fedha **2023/24 (Januari 2024)** ambapo jumla ya **wanafunzi 656** walipata mafunzo na kufaulu. Hadi kufikia mwaka wa fedha **2025/26 (Juni 2026),** jumla ya **wanafunzi 7,216** walipata mafunzo na kufaulu kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 03:

**Jedwali Na. 03: Vyuo vya Mafunzo na Idadi ya Wahudumu Waliopata Mafunzo**

| Na. | Jina la Chuo | Kuanza Mafunzo | Idadi ya Wahudumu Waliopata Mafunzo | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | Jumla |
| 1. | Vocational Education and Training Authority (VETA) | Aprili 2026 | - | - | 93 | **93** |
| 2. | Arusha Technical College (ATC) | Aprili 2026 | - | 169 | 793 | **962** |
| 3. | National Institute of Transport (NIT) | Februari 2024 | 508 | 1,051 | 1,914 | **3,473** |
| 4. | College of Business Education (CBE) | Januari 2024 | 148 | 1,483 | 1,057 | **2,668** |
| **Jumla** | | | **656** | **2,703** | **3,857** | **7,216** |

***Chanzo:*** *LATRA, 2026*

Wahudumu waliohitimu na kufaulu mafunzo ya uhudumu, hupaswa kuwasilisha maombi ya kusajiliwa LATRA kwa njia ya Mfumo wa TEHAMA (RRIMS). Idadi ya wahudumu waliowasilisha maombi na kusajiliwa LATRA iliongezeka kutoka 137 (21%) mwaka wa fedha 2023/24, hadi 2,956 (77%) mwaka 2025/26. Kwa ujumla, wahudumu waliosajiliwa LATRA hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2025/26 ilifikia 4,664 (65%) kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 04:

**Jedwali Na. 04: Idadi ya Wahudumu Waliopata Mafunzo na Kusajiliwa**

| Na. | Aina ya Vipindi | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Waliofapata Mafunzo ya Uhudumu | 656 | 2,703 | 3,857 | **7,216** |
| 2 | Waliosajiliwa LATRA na Kupatiwa Kadi | 137 | 1,571 | 2,956 | **4,664** |
| 3 | Kiwango cha Ufaulu | 21% | 57% | 77% | **65%** |

***Chanzo:*** *LATRA, 2026*

### 4.1.3 Usajili na Uidhinishwaji wa Mifumo ya Teksi Mtandao

LATRA imeendelea kusajili na kuidhinisha wamiliki na waendesha mifumo ya teksi mtandao katika nchi yetu. Hadi kufikia mwaka 2026 kampuni **22** zimesajiliwa na kuidhinishwa kutoa huduma ya kuwaunganisha wasafirishaji wenye magari ya kutoa huduma za teksi mtandao wapatao **23,532** ambao wana leseni hai za kutoa huduma za usafiri kwa njia ya mtandao kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 05.

**Jedwali Na. 05: Idadi ya Leseni za Mifumo ya Teksi Mtandao**

| Aina ya chombo | Idadi ya Leseni |
|---|---|
| Teksi mtandao (Pikipiki Magurudumu mawili) | 11,407 |
| Teksi mtandao (Pikipiki Magurudumu matatu) | 8,083 |
| Teksi (Magari) | 4,042 |
| Jumla | **23,532** |

***Chanzo:*** *LATRA, 2026*

### 4.1.4 Kutumia Mawakala Kutoa Leseni za Magari ya Kukodi

Mwaka 2023, Serikali ilifanya marekebisho ya Kanuni za LATRA za Huduma za Magari ya Kukodi, 2020 (GN No. 78 la tarehe 07/02/2020), kwa kuruhusu Mwakala (Authorized Agents) wa aina nne (4): Kampuni, Vyama vya Ushirika, Taasisi za Umma, na Watu Binafsi kutoa leseni za LATRA kwa vyombo vya usafiri wa kukodi. Katika kipindi cha miaka mitatu ya utekelezaji wa marebisho haya ya Kanuni, kuanzia mwaka wa fedha 2023/24 hadi 2025/26, **LATRA iliweza kutoa Vyeti kwa Mawakala 100** ilijumuisha **Kampuni-69**, **Vyama vya Ushirika-7, Taasisi za Umma (LGAs na Shirika la Posta Tanzania)-23, na Mtu Binafsi-1.** Mawakala hawa waliweza kutoa asilimia 70 ya leseni za Pikipiki, kukusanya jumla ya **Shilingi Bilioni 7.9,** kulipwa **Kamisheni Shilingi Bilioni 2.0** kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 06.

**Jedwali Na. 06: Idadi ya Wahudumu Waliopata Mafunzo na Kusajiliwa**

| Na. | Maelezo | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| | | TZS '000' | TZS '000' | TZS '000' | TZS '000' |
| **1.0** | **Mapato - Mawakala:** | | | | |
| 1.1 | Mawakala - Sekta ya Umma (LGAs & Shirika la Posta) | 1,430,736 | 670,304 | 480,499 | **2,581,539** |
| 1.2 | Mawakala – Sekta Binafsi | 8,469 | 419,709 | 4,874,900 | **5,303,078** |
| **1.3** | **Jumla ya Mapato** | **1,439,205** | **1,090,013** | **5,355,399** | **7,884,617** |
| | | | | | |
| **2.0** | **Kamisheni -Mawakala** | | | | |
| 2.1 | Mawakala - Sekta ya Umma (LGAs) | **715,368** | **134,061** | **96,100** | **945,529** |
| 2.2 | Mawakala – Sekta Binafsi | **1,694** | **83,942** | **974,980** | **1,060,616** |
| **2.3** | **Jumla ya Kamisheni** | **717,062** | **218,003** | **1,071,080** | **2,006,144** |

***Chanzo:*** *LATRA, 2026*

### 4.1.5 Utekelezaji wa Mfumo wa Tiketi Mtandao (e-Ticketing) kwa Mabasi

LATRA ilianza kutekeleza Mfumo wa Tiketi Mtando mwaka wa fedha 2022/2023. Aidha, kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA), na Shirika la Reli Tanzania (TRC), LATRA ilikamilisha na kuanza kutekeleza mfumo wa Tiketi Mtandao (Core e-Ticketing System-CeTS) inayoweka mabasi yaendayo mikoani na Nchi Jirani kwenye mfumo huo, yaani, **Stendi Kiganjani**. CeTS inamwezesha abiria kukata tiketi za mabasi na treni za TRC kupitia **Safari Tiketi App** inayopatikana kwenye mitandao ya simu za *Android* na *iOS* au kupitia tovuti tiketi.latra.go.tz. Mfumo wa CeTS umeunganisha mifumo ya tiketi ya watoa huduma za usafiri wa umma ikiwemo mabasi, treni za TRC (MGR na SGR).

Kufikia mwezi Juni 2026, LATRA ilikuwa na **watoa huduma 14 wa Tiketi Mtandao** ambao mifumo yao imeunganishwa na LATRA. Watoa huduma hao ni **Busbora Company Limited, Otapp Agency Company Limited, Abood Bus Service Limited, Duarani Innovate Limited, Shabiby Transporters, Hashtech Tanzania Limited, Iyishe Company Ltd, Voltic Tanzania Limited, Web Corporation Tanzania Limited, Mkombozi Infotech Company Limited, Itule Company Limited, Sepa Tech Limited, Logix Co Limited, na Global Light & Company Limited.** Pamoja na mchango wao kwenye kuboresha huduma za usafiri wa abiria, wapo ambao wameonekana kutumia mifumo yao ya kuwasilisha taarifa zenye mashaka LATRA. Mamlaka inaendelea na ufuatiliaji na itachukua hatua stahiki za udhibiti itakapobidi.

Kwa ujumla, utekelezaji wa Mfumo wa Tiketi Mtandao umeboresha huduma kwa abiria kujikatia tiketi popote alipo, kuchagua muda wa kusafiri (usiku au mchana), kuchagua basi na daraja la basi analotaka, kisha hulipa nauli kwa njia ya mtandao (online) au taslimu (cash) anapokuwa kwenye ofisi za mawakala au kampuni husika. Idadi ya abiria na miamala iliyofanyika kwa kipindi cha utekelezaji wa mfumo huu imekuwa ikiongezeka kutoka **abiria 7,112** na miamala ya **Shilingi Bilioni 226.29** mwaka 2022/23**,** hadi **abiria 28,673** na miamala ya **Shilingi Bilioni 993.96** mwaka 2025/26 kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 07.

**Jedwali Na. 07: Idadi ya Abiria Waliosafiri na Miamala yao kwa 2022/23-2025/26**

| Mwaka wa Fedha | Idadi ya Abiria (Cash) ('000') | Idadi ya Abiria (Online) ('000') | Jumla ya Abiria Wote ('000') | Nauli zilizolipwa - Cash (Sh. Mil.) | Nauli zilizolipwa - Online (Sh. Mil.) | Jumla ya Malipo yote ya Nauli (Sh. Mil.) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2022/2023 | 7,072 | 40 | **7,112** | 224,638 | 1,649 | **226,287** |
| 2023/2024 | 5,969 | 87 | **6,056** | 185,792 | 4,537 | **190,329** |
| 2024/2025 | 19,484 | 858 | **20,342** | 679,756 | 41,287 | **721,043** |
| 2025/2026 | 26,746 | 1,927 | **28,673** | 897,147 | 96,809 | **993,956** |
| **Jumla** | **59,271** | **2,912** | **62,183** | **1,987,333** | **144,282** | **2,131,615** |

***Chanzo:*** *LATRA, 2026*

Tathmini ya takwimu zilizo kwenye Jedwali Na. 06 inaonesha kwamba **abiria wengi wamekuwa wakilipa nauli kwa fedha tasilimu na wachache wamekuwa wakilipa kwa njia ya mtandao (online).** Hivyo, katika kipindi cha miaka minne (4) ya utekelezaji wa matumizi ya mifumo ya Tiketi Mtandao, kati ya **abiria Milioni 62.18** waliotumia mifumo hiyo, **abiria Milioni 59.27 sawa na asiimia 95.3** walilipa nauli zao kwa **fedha taslimu (cash)** na **abiria Milioni 2.91 sawa na asilimia 4.7** walilipa nauli zao kwa **njia ya mtandao (online).** Aidha, kwa upande wa jumla ya malipo yote ya nauli ya **Shilingi Trilioni 2.13**, kiasi cha malipo ya **Shilingi Trilioni 1.99 sawa na asilimia 93.2** yalifanywa kwa **fedha taslimu (cash)** na malipo ya **Shilingi Bilioni 144.28 sawa na asilimia 6.8** yalifanywa kwa **njia ya mtandao (online).**

### 4.1.6 Usimamizi wa Usafiri wa Mabasi Usiku na Mchana (24/7)

Uamuzi wa kuruhusu mabasi ya masafa marefu kufanya safari kwa saa 24 ni moja ya mageuzi makubwa ya huduma za usafiri wa barabara. Katika mwaka wa fedha 2022/23, Serikali iliruhusu mabasi kusafiri usiku na mchana (24/7) na hivyo kuongeza

muda wa safari kwa baadhi ya waendeshaji waliokidhi masharti. Kuanzia tarehe 1 Oktoba 2023, utoaji wa ratiba za saa 24 ulianza rasmi.

Uamuzi huu uliwezekana kwa kuimarika kwa usalama, miundombinu, mifumo ya mawasiliano na uwezo wa LATRA kufuatilia mabasi kwa Mfumo wa Ufuatiliaji wa Magari (VTS). Masharti ya usalama yalijumuisha madereva kuthibitishwa na LATRA, na kutumia vitufe vya utambuzi wa madereva (i-buttons) kuwezesha ufuatiliaji wa mwenendo wa mabasi na madereva wanapokuwa barabarani. Katika mwaka wa fedha 2024/25, LATRA ilifanya tathmini ya usafiri wa mabasi wa 24/7, na kubaini kuwa huduma hii safari za usiku zimepunguza msongamano kwenye stendi, zimepungusha ushindani wa mabasi kusafiri kwa mwendokasi hatarishi, na abiria wengi wamekuwa wakipendelea kusafiri usiku kwa kuwa imepunguza sana au kuondoa kabisa uhitaji wa kugharamia malazi, hususan kwa wafanyabiashara.

Kwa ujumla, kwa abiria, safari za mabasi kwa 24/7 zimeongeza chaguo la muda wa kusafiri, kuwapunguzia gharama za malazi kwa kusafiri usiku na kutumia muda wa mchana kwa shughuli za uzalishaji. Aidha, kwa watoa huduma, safari za 24/7 zimeongeza faida, uwekezaji, na fursa za biashara. Kwa upande wa LATRA, safari za 24/7 zimeongeza ufanisi wa matumizi ya miundombinu ya barabara na stendi, wajibu wa kuhakikisha uchovu wa madereva, mwendokasi, hali ya magari na uzingatiaji wa ratiba vinadhibitiwa kwa karibu.

## 4.2 Udhibiti Usafiri wa Reli

### 4.2.1 Udhibiti wa Usalama wa Huduma za Reli

LATRA imeendelea na jukumu lake la udhibiti wa huduma za reli unaojumuisha **usalama wa miundombinu na vitembeareli, nauli, viwango vya ubora na ufanisi wa utendaji**. Katika hatua ya kutimiza majukumu haya, LATRA katika kipindi kinachoanzia mwaka wa fedha 2021/22 hadi 2025/26 **imefanya jumla ya kaguzi 275 katika miundombunu, ishara na mawasiliano**, **vitembea reli** (vichwa na mabehewa) **na uendeshaji.** Kati ya kaguzi hizi, **143 zilikuwa kwa Shirika la Reli Tanzania (TRC), na kaguzi 132 zilikuwa kwa Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA)**.

### 4.2.2 Utoaji wa Leseni za Uendeshaji wa Reli

LATRA ilitekeleza jukumu la kisheria chini ya Kifungu cha 5(1)(b) kwa kutoa leseni za uendeshaji wa reli kwa Mashirika ya TRC na TAZARA Revitalization Limited (Kampuni tanzu iliyopewa Mkataba wa Uendeshaji wa TAZARA) kupitia uwekezaji wa China kwenye Reli ya TAZARA. Kampuni hiyo iliyo chini ya CCECC (China Civil Engineering Construction Company) imeingia mkataba na Serikali za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Zambia kukarabati na kuendesha reli ya TAZARA kwa kipindi cha miaka 30 kuanzia mwaka 2025. Pia Mamlaka ilitoa leseni za uendeshaji kwa watoa huduma binafsi wa TAZARA kwa makampuni ya Calabash Limited na Bravo Group.

### 4.2.3 Usimamizi Usalama na Ufuatiliaji Huduma za SGR

Katika uendeshaji wa huduma za usafiri wa abiria kwa treni za SGR, LATRA imetekeleza jukumu la **kuthibitisha ubora wa vitembeareli** kabla ya kuanza kutoa huduma na kuthibitisha utayari wa miundombinu kwa ajili ya kutoa huduma bora na salama. LATRA ilithibitisha ubora wa vitembeareli kwenye SGR kwa mujibu wa Sheria ya Reli Sura 170 (Iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2023). **Jumla ya vichwa vya treni 17 (vipya)**, **Mabehewa mapya ya abiria 56 (kutoka Korea Kusini)**, **treni za seti za umeme (EMU) 10 (Korea Kusini), Injini 8 za aina ya 91 za TRC (Malaysia)** na **Mabehewa 264 ya mizigo (Kutoka China)** yalipewa ithibati ya ubora na kuanza kutoa huduma kwa umma. Pia Mamlaka ilifanya kaguzi za kuthibitisha ubora wa vitembeareli kwa wawekezaji binafsi wa TAZARA ikiwemo African Inland Logistics na Bravo Group kwa mabehewa (yaliyokarabatiwa) jumla yalikuwa 68 na pia injini tatu (3) za dizeli zilizokarabatiwa nchini Afrika Kusini.

### 4.2.4 Upangaji wa Nauli za Treni za SGR

Katika mwaka wa fedha 2023/2024, LATRA ilitekeleza jukumu la kisheria chini ya Kifungu cha 5(1)(c) kwa kupanga nauli za Daraja la Uchumi (Economy Class) wakati wa kuanzishwa kwa huduma za treni za kisasa (SGR). Kwa mujibu wa kifungu cha 19 cha Sheria ya LATRA, Bodi ya Wakurugenzi ya LATRA iliidhinisha nauli za abiria kwa daraja la uchumi (economy class) kwa treni inayosimama kila kituo (ordinary train) na treni inayosimama katika vituo maalum (express train) na nauli hizo kuanza kutumika mwezi Juni 2024.

**Nauli za Treni ya SGR zilitangazwa kupitia Taarifa ya Kawaida Na 8931 kwenye Gazeti la Serikali Toleo Na. 24 la 14 Juni 2024** zikiwa ni Shilingi 31,000 kwa treni ya kawaida (inayosimama kila kituo) na Shilingi 50,000 kwa treni inayosimama vituo maalum (express) kati ya Dar-es-Salaam na Dodoma. Nauli zilizoidhinishwa zimeelekeza mtoto mwenye umri kuanzia miaka minne hadi miaka 12 kutozwa nusu ya nauli na mtoto mwenye umri chini ya miaka minne kutotozwa nauli. Aidha, **LATRA iliruhusu TRC kujipangia nauli za SGR kwa Daraja la Biashara (Business Class) na madaraja mengine ya juu (Royal Class)** kwa kuwa eneo hili ni kwa abiria wenye uwezo kifedha na wanaoweza kufikia huduma hii.

### 4.3 Udhibiti Usafiri wa Waya (Cable Transport Regulation)

Serikali ya Awamu ya Sita kupitia Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa (2021/2022 hadi 2025/2026) imeweka msisitizo katika kuboresha huduma za utalii nchini. Katika kutekeleza jukumu hili, LATRA imefanya utambuzi wa mahitaji, utayari wa wadau, na maeneo ya uwekezaji nchini. **Tathmini ya awali ya LATRA** imebainisha maeneo yenye vivutio yaliyopo kwenye mikoa nane (08) ya **Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Iringa, na Mbeya.**

Aidha, rasimu ya Kanuni za Udhibiti wa Usafiri wa Waya zilishaandaliwa na Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikisha wadau. Kanuni hizo zilijadiliwa kwenye kikao cha Wadau kilichofanyika tarehe 23 Disemba 2024. Pia, Bodi ya LATRA kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina, Wizara ya Uchukuzi, na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, imekamilisha mapitio ya Muundo wa Uongozi na Mgawanyo wa Majukumu na kuunda Kitengo cha Udhibiti Usafiri wa Waya na kuwezesha usimamizi wa Kanuni za Usafiri wa waya, pindi zitakapokamilika na kuidhinishwa na Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi kwa mujibu wa Kanuni ya 45 ya Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Sura ya 413.

### 4.4 Kukuza matumizi ya TEHAMA kwenye utoaji wa huduma

#### 4.4.1 Mfumo wa Usimamizi wa Shughuli za Kiudhibiti (RRIMS)

LATRA imeendelea kuzingatia ubunifu hususan katika matumizi ya TEHAMA kwenye utekelezaji wa majukumu yake. Katika kipindi cha utendaji wake, LATRA imejenga mfumo wa TEHAMA unaojulikana kama Railway and Road Information Management System (RRIMS) ambao ni mfumo mkuu wa utoaji leseni, usajili madereva, malipo na taarifa za udhibiti. Mfumo wa **RRIMS umeunganishwa na mifumo ya taasisi**

**nyingine za Serikali** kama vile **TRA, TIRA, NIDA, GePG, Polisi (VIR), na BRELA** ili kurahisisha uhakiki wa nyaraka. Aidha, **Mfumo wa RRIMS unamwezesha msafirishaji kufanya maombi ya leseni na huduma zake pamoja na kuchapa leseni iliyoidhinishwa ndani ya saa 24 bila kuhitaji kufika ofisi za LATRA**, na hivyo kupunguza kwa kiwango kikubwa usumbufu na muda wa kupata huduma.

### 4.4.2 Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTS)

LATRA ilirithi kutoka SUMATRA na kufanyia maboresho Mfumo wa Kufuatilia mwenendo wa Magari (Vehicle Tracking System – VTS) unaotumia 'Satelite', VTS imeunganishwa na Kifaa cha Kufuatilia Mwenendo wa Magari (VTD), Mtandao wa Mawasiliano na Vifaa vya Uhifadhi wa Taarifa (GPS Data Servers) vinavyofanya kazi kwa pamoja na kutuma taarifa za mwenendo mzima wa mabasi kwenda kituo cha ufuatiliaji (VTS Monitoring Center). Mfumo huu unalenga kusimamia matakwa ya usalama wa huduma kama ilivyoelekezwa kwenye Kifungu cha 5(1)(d) na Kifungu cha 6(g) cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Sura ya 413, LATRA. Idadi ya magari (mabasi) yaliyounganishwa na VTS imekuwa ikiongezeka kutoka **mabasi 5,979 mwaka wa fedha 2021/22** hadi kufikia **mabasi 14,743 mwaka wa fedha 2025/26** kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 08.

**Jedwali Na. 08: Idadi ya magari yaliyounganishwa VTS**

| S/n | Mwaka wa Fedha | Idadi ya Magari Yote |
|---|---|---:|
| 1 | 2021/2022 | 5,979 |
| 2 | 2022/2023 | 7,626 |
| 3 | 2023/2024 | 9,951 |
| 4 | 2024/2025 | 11,836 |
| 5 | 2025/2026 | 14,743 |

***Chanzo:*** *LATRA, 2026*

Aidha, **vichwa 27 vya treni** zinaotoa huduma za usafirishaji mizigo kwenye reli ya TAZARA vimeunganishwa kwenye mfumo wa VTS. Vilevile, VTS imewezesha utambuzi wa madereva waliothibitishwa wakiwa barabarani kwa kutumia vitufe vya utambuzi (i-buttons). Idadi ya madereva waliopewa *i-buttons* imeongezeka kutoka **madereva 256 mwaka wa fedha 2022/23** ambapo utaratibu wa matumizi ya *i-buttons* ulianza hadi kufikia **madereva 13,829 mwaka wa fedha 2025/26**, kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na. 09.

**Jedwali Na. 09: Vitufe vya Utambuzi (i-button) wlizopewa madereva**

| S/N | Mwaka wa Fedha | Vitufe Vilivyogawiwa kwa Madereva |
|---|---|---|
| 1 | 2022/2023 | 256 |
| 2 | 2023/2024 | 1,797 |
| 3 | 2024/2025 | 6,119 |
| 4 | 2025/2026 | 13,829 |

***Chanzo:*** *LATRA, 2026*

### 4.4.3 Mfumo Tumizi wa LATRA (LATRA App)

LATRA imeendelea kutekeleza mfumo tumizi unaopatikana kwenye simujanja kupitia 'Play Store' kwa simu za *Android* na "App Store" kwa simu za *"iPhone (Apple)"* . Huduma hii inamuwezesha mwananchi kupata taarifa za nauli za mabasi, kutambua uhalali wa leseni za magari na adhabu, hivyo kumuwezesha abiria kuepuka kutumia gari lenye changamoto ili kujiepusha na usumbufu. Aidha kutumia LATRA App mwananchi anaweza kupata taarifa za mwenendo wa basi lolote na taarifa ya mabasi yanayowasili katika vituo vya mabasi nchini. Kupitia LATRA App pia mawakala wanaweza kutoa leseni za LATRA kwa Pikipiki za miguu mitatu na miwili.

### 4.4.4 Mfumo wa Taarifa kwa Abiria (Passenger Information System -PIS)

LATRA imetengeneza Mfumo wa Taarifa kwa Abiria (Passenger Information System -PIS) unaomuwezesha mwananchi kutambua muda ambao basi la masafa marefu litafika katika stendi ya mabasi aliyoichagua pamoja na kufahamu mwendo wa basi husika pindi akiwa safarini. Kwa sasa mfumo wa PIS upo katika runinga zilizofungwa kwenye stendi ya mabasi Magufuli Dar es Salaam na stendi ya mabasi nanenane jijini Dodoma, lakini pia mfumo huo unapatikana kwa anwani ya pis.latra.go.tz kupitia simu janja au komputa.

### 4.4.5 Matumizi ya Mfumo wa e-Mrejesho

LATRA imeendelea kutumia Mfumo wa Serikali wa e-Mrejesho unaotumika kwa ajili ya kupokea Malalamiko, Mapendekezo, Pongezi au Maulizo. Mfumo unapatikana kwa anwani ya emrejesho.gov.go.tz au kwa kupakua mfumo tumizi wa e-Mrejesho au kwa kutumia simu kwa njia ya msimbo (USSD) au kwa kupitia tovuti ya LATRA www.latra.go.tz sehemu ya tovuti mashuhuri. Hivyo, tunawasihi wananchi wote kutumia mfumo huo na tunawahakikishia kushughulikia masuala yatakayowasilishwa ndani ya siku 21 tangu watakapowasilisha lalamiko au maulizo yao.

### 4.5 Elimu kwa Umma na Maonesho

#### 4.5.1 Uandaaji na Urushaji wa Vipindi vya Elimu kwa Umma

LATRA kupitia studio yake iliyoko Dar es salaam imeendelea kuandaa maudhui na vipindi vya elimu kwa umma; na kuvirusha kupitia Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC1), Clouds TV na mitandao ya kijamii kama vile 'LATRA Online TV' (You tube, Instagram, Facebook na X). Aidha, katika kipindi cha miaka mitano (5) ya taarifa hii, LATRA iliandaa na kurusha **vipindi 649**, ambapo **vipindi 256 vilirushwa kwa runinga (TV)**, na **vipindi 393 vilirushwa kupitia mitandao ya kijamii**. Jedwali Na 10 linaonesha taarifa ya vipindi vilivyoandaliwa na kurushwa katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022 hadi 2025/2026.

**Jedwali Na 10: Vipindi vya Televisheni na Mitandao ya Kijamii, 2020/21-2025/26**

| Na. | Aina ya Vipindi | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Vipindi vya Runinga (TV) | 48 | 52 | 52 | 52 | 52 | **256** |
| 2 | Mitandao ya Kijamii | 30 | 63 | 68 | 126 | 106 | **393** |
| | **Jumla** | **78** | **115** | **120** | **178** | **158** | **649** |

***Chanzo:*** *LATRA, 2026*

Aidha, kufuatia elimu inayotolewa kwa wananchi kupitia mitandao ya kijamii, LATRA imeendelea kupata wafuasi kwenye mitandao hiyo wanaofuatilia na kupata taarifa na elimu zaidi kuhusu huduma za usafiri ardhini.

#### 4.5.2 Maadhimisho ya Kwanza ya Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini, 2025

Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikiana na LATRA pamoja na wadau wa usafiri ardhini ilipanga na kufanya Maadhdimisho ya Kwanza ya Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini, 2025, tarehe 24 hadi 29 Novemba 2025, yenye Kauli Mbiu ***Nishati Safi na Ubunifu katika Usafirishaji (Green Transport and Innovation),*** sambamba na **Siku ya Usafiri Endelevu Duniani tarehe 26 November, 2025**. Katika maadhisho hayo, Mgeni Rasmi alikuwa Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maadhimisho yalihusisha Makongamano katika ukumbi huu wa JNICC na Maonesho yaliyohusisha wadau wa sekta ya usafiri ardhini ndani na nje ya nchi yaliyofanyika viwanja vya Mnazi mmoja, Dar es Salaam ambazo zaidi ya wadau 1,200 wa kitaifa na kimataifa walishiriki kwenye makongamano na huku waoneshaji 60 wa kitaifa na kimataifa wakitoa huduma wakati wa maonesho. Maadhimisho hayo yaliambatana na tuzo mbalimbali walizopatiwa

wasafirishaji waliofanya vizuri kwa kutekeleza majukumu yao kwa kufuata mashari ya leseni walizopatiwa na kutii Sheria, Kanuni na Taratibu za sekta ya usafirishaji nchini.

LATRA imeendelea kushiriki kwenye maonesho mbalimbali ya Kitaifa na Kisekta kwa lengo la kutoa elimu kwa wananchi, yakiwemo maonesho ya **Sabasaba, Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani Tanzania Bara**, **Maonesho ya Nanenane**, **Wiki ya Usalama Barabarani Zanzibar**, **Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma** na **Mkutano wa Mwaka wa Sekta ya Uchukuzi**. Katika kipindi cha miaka miwili mfululizo, LATRA imetambulika kwa jitihada za kutoa elimu kwa umma na kupewa tuzo mbalimbali katika maonesho haya.

### 4.5.3 Huduma kwa Wateja

LATRA imeanzisha kituo cha huduma kwa wateja mwaka 2023/24 kinachofanya kazi kwa saa zote ili kurahisisha utatuzi wa migogoro na changamoto kwa wakati. Huduma za kituo hicho zinapatikana kupitia namba za kupiga bila malipo **0800110019** na **0800110020**. Aidha LATRA imeendelea kuzitangaza namba hizi kupitia vipindi vya elimu kwa umma, mitandao ya kijamii na kuzibandika katika maeneo mbalimbali yanayofikiwa na wadau wetu. Kwa sasa, namba hizi zinaandikwa kwenye milango ya mabasi ya mijini sambamba na viwango vya nauli.

## 5.0 TAARIFA MUHIMU KWA UMMA NA WADAU WA USAFIRI ARDHINI

**Ndugu Wanahabari,** ninapoelekea kumalizia wasilisho langu, naomba kutoa taarifa muhimu nne (4) kwa Umma na wadau wa usafiri ardhini kama ifuatavyo:

### 5.1 Maadhimisho ya Pili ya Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini, 2026

LATRA inapenda kuuarifu Umma na wadau wa usafiri ardhini kuanza kwa maandalizi ya Maadhimisho ya Pili ya Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini, 2026. Maadhimisho haya yamepangwa kufanyika katika ukumbi wa **Mlimani City, Barabara ya Sam Nujoma, Dar es Salaam, kwa siku tatu (3), kuanzia tarehe 24 hadi 26 Novemba, 2026,** samababmba na **Siku ya Usafiri Endelevu Duniani, tarehe 26 Novemba 2026.** Aidha, maadhimisho hayo yataambatana na maonesho ya bidhaa na huduma zinazohusika katika mnyororo wa thamani wa usafiri ardhini, na inatarajiwa kuwa na **washiriki takriban 2,000 kutoka ndani na nje ya Tanzania.**

Kauli Mbiu ya Maadhimisho ya Wiki ya Usafiri Endelevu Ardhini, 2026 itakuwa ***Kuharakisha Usafiri Endelevu: Usafiri Salama, Rafiki kwa Mazingira na Jumuishi kwa Wote*** **(***Accelerating Sustainable Transport: Safe, Green and Inclusive Mobility for All*). Lengo ni kuleta wadau wa sekta ya uchukuzi na wanachi kwa ujumla, kujielimisha, kujadili na kuweka mikakati ya pamoja ya kuboresha sekta ya usafiri ardhini na kuchochea ukuaji wa shughuli za kijamii na kiuchumi.

Hivyo, tunawakaribisha wadau kushiriki katika maadhimisho haya kwa kufanya maonesho katika viwanja vya Mlimani City na kushiriki katika makongamano kwa utaratibu utakaotangazwa siku chache zijazo.

### 5.2 Fursa kwa Wasafirishaji Wakati wa Mashindo ya AFCON, 2027

Mwaka 2027, Tanzania, pamoja na Kenya na Uganda, tutakuwa wenyeji mashindano ya AFCON 2027 (**PAMOJA AFCON 2027)**. Hii itakuwa mara ya kwanza katika historia ya AFCON kwa mashindano hayo kuandaliwa kwa pamoja na nchi tatu za Africa Mashariki. CAF inatarajia mashindano haya kuvutia **zaidi ya mashabiki milioni 1.5** katika nchi hizi tatu na nchi za Afrika.. Hii ni fursa kwa wasafirishaji kwa kuwa **abiria wataongezeka, Watalii wataongezeka, Wageni wataongezeka.** Mahitaji ya usafiri kwa ujumla yataongezeka kwa ajili ya kuwapeleka mashabiki katika maeneo ya viwanja vya mashindano, kutoka mijini, mikoa mbalimbali na nchi jirani zenye mashabiki wengi wa mpira wa miguu kuelekea katika mkoa wa Dar es Salaam, Arusha na Zanzibar na mikoa/miji jirani. **LATRA kupitia utaratibu wa mawasiliano kwa umma tumeendelea kuwahabarisha wadau wetu juu ya fursa za zabuni za huduma ya usafiri zilizotangazwa CAF** kupitia tovuti yao https://www.cafonline/inside-caf/about-us/official-documents/tenders/afcn

Kwa ujumla, ujio wa AFCON 2027 ni fursa kwa watoa huduma za usafiri wa umma na usafiri wa kukodi kuongeza vipato. Aidha, ni fursa kubwa sana kwa hoteli, migahawa, mikahawa, wafanyabiashara, waongoza watalii, na wananchi kwa ujumla kufanya shughuli za kijamii na kiuchumi ziwe bora Zaidi. Hivyo, **AFCON 2027 si mpira pekee. Ni biashara, ni utalii, ni usafiri, ni ajira na ni fursa ya kuitangaza Tanzania.** Swali muhimu kwa wadau wa sekta ya uchukuzi na watanzania kwa ujumla ni: ***Tufanye nini ili mgeni anayekuja Tanzania wakati wa AFCON 2027 aondoke akiwa na kumbukumbu nzuri na atamani kurudi tena?***

**Jibu ni rahisi lakini linahitaji nidhamu**: *Tuwapokee vizuri. Tuwahudumie vizuri. Tuwape usafiri salama. Tuwaheshimu. Tusiwatoze bei za dhuluma. Tusiwabague kwa sababu ni wageni. Tuwasaidie wanapohitaji maelekezo. Magari yetu yawe safi. Madereva wetu wawe nadhifu, wastaarabu na wenye lugha nzuri. Tuwe waaminifu kwa mali za abiria. Tuwe wakarimu na ikiwezekana, tubalidilishane nao mawasiliano.* Tukifanya haya, pamoja na mengine mengi mazuri tutakayoelekezwa na viongozi wetu, ili tuwe mabalozi wa kweli wa Tanzania. Napendekeza kila dereva ajiulize: **"Mgeni huyu akiondoka Tanzania, atasimulia nini kuhusu mimi na Nchi yangu?"** Tukifanya vizuri, atasema: **"Tanzania ni Nchi nzuri. Watu wake ni wakarimu. Madereva wake ni waaminifu, na Huduma zao ni nzuri. Nitarudi tena."** *Hiyo ndiyo Tanzania tunayoitaka*, na maandalizi yake yanapaswa kuanza leo, sio Mwaka 2027.

### 5.3 Amri ya Waziri wa Fedha ya Miamala ya Kielektroniki, 2026

LATRA inapenda kuuarifu Umma na wadau wa usafiri ardhini kuanza kutumika kwa **Amri ya Miamala ya Kielektroniki (Malipo ya Lazima kwa Njia za Kielektroniki kwa Miamala Iliyoainishwa), 2026**, iliyotolewa na Waziri wa Fedha chini ya **kifungu cha 13(2)** cha **Sheria ya Miamala ya Kielektroniki, Sura ya 442**. Amri hiyo imeanza kutumika tarehe **1 Julai 2026** na inataka malipo yanayohusiana na miamala iliyoainishwa katika Jedwali lake kufanyika au kupokelewa kupitia njia za kielektroniki. Kwa kuzingatia majukumu ya Mamlaka katika kusimamia na kudhibiti huduma za usafiri ardhini, LATRA inaukumbusha Umma na wadau wa usafiri ardhini kuisoma, kuielewa, na kuzingatia matakwa ya Amri hiyo, hususan kwa miamala ya usafiri ardhini. Miamala hiyo ni pamoja na **malipo ya ada, tozo, ushuru; malipo ya nauli zinazohusiana na huduma za mabasi yaendayo haraka (BRT), vivuko, madaraja, mabasi ya abiria ya masafa marefu, teksi mtandao, usafiri wa reli na huduma za maegesho**. Malipo mengine yanayopaswa kufanywa kwa njia ya kielekroniki ni yanayofanywa katika **vituo vya kujaza mafuta;** malipo ya **malazi, chakula na vinywaji katika hoteli, migahawa na mikahawa;** malipo yanayohusiana na **huduma za utalii;** na malipo ya **kuuza au kununua magari.**

### 5.4 Tahadhari Kuhusu Mvua Kubwa za El Nino

Tunawataarifu wadau wote wa sekta ya usafiri ardhini, wakiwemo wamiliki wa vyombo vya moto kibiashara, madereva, abiria na watoa huduma za usafiri ardhini, kuchukua tahadhari kabla, wakati na baada ya safari katika kipindi cha mvua za El Niño kwa

kufuatilia taarifa rasmi za hali ya hewa na kuzingatia maelekezo ya mamlaka husika kuhusu hali ya barabara na usalama wa safari.

Mvua hizo zinaweza kusababisha mafuriko, maji kuvuka barabara, utelezi, mmomonyoko na maporomoko ya udongo au mawe, kuharibika kwa barabara, upepo mkali na ukungu unaopunguza uono, hali zinazoweza kuhatarisha usalama wa safari. Katika kipindi chote cha mvua, Wamiliki wa vyombo vya usafiri wanapaswa kuhakikisha vyombo vyao vinakaguliwa na kufanyiwa matengenezo ya mara kwa mara, hususan mifumo ya breki, matairi, taa, vioo na visafisha vioo (wipers), na hitilafu zote kurekebishwa kabla ya safari. Pia, safari zipangwe kwa kuzingatia hali ya hewa na barabara na madereva wapewe maelekezo ya tahadhari.

Aidha, madereva wanapaswa kuepuka kuvuka maeneo yenye maji yanayotiririka kwa kasi au kina kisichojulikana; kupunguza mwendo na kuongeza umbali wakati wa mvua, ukungu au uono hafifu; kuwa makini katika maeneo yenye maporomoko, mmomonyoko, nyufa au kingo zilizoathirika; na kuepuka kusimama au kuegesha katika maeneo hatarishi. Watumie taa ipasavyo na wazingatie alama za barabarani na maelekezo ya mamlaka. Endapo hali si salama, safari isitishwe au iahirishwe.

Kwa upande wa abiria wanashauriwa kufuatilia taarifa za hali ya hewa na barabara kabla ya safari, kuepuka safari zisizo za lazima wakati wa mvua kubwa, kujiandaa mapema, na kutoa taarifa kwa mamlaka kuhusu ukiukwaji wa usalama kama mwendo kasi, uzidishaji wa abiria au uendeshaji usio salama. Pia washirikiane na madereva na wahudumu na kuzingatia maelekezo ya usalama. Nao wamiliki na madereva wa magari ya shule waweke usalama wa wanafunzi mbele kwa kupanga safari kwa kuzingatia hali ya hewa, barabara na uono wa dereva, na kuepuka maeneo yenye mafuriko, utelezi mkubwa au maji yanayotiririka kwa kasi. Endapo hali si salama, safari isitishwe au iahirishwe.

LATRA inawahimiza wadau wote kuwa makini, kuzingatia maelekezo ya mamlaka husika na kuweka usalama mbele katika kila safari. Ukibaini hali hatarishi au tukio linaloweza kuathiri usalama wa usafiri, piga simu LATRA saa 24 bila malipo 0800110019 au 0800110020, au tuma ushahidi WhatsApp 0681300800 ili hatua stahiki zichukuliwe kwa wakati.

## 6.0 HITIMISHO

**Ndugu Wanahabari,** naomba nihitimishe wasilisho langu kwa kuwafahamisha kwamba mwaka huu wa fedha 2026/2027 LATRA imejipanga **kuhakikisha kuwa huduma za usafiri ardhini zinakuwa bora na salama zaidi, zinawafikia wananchi, kuondoa kero na changamoto mbalimbali katika sekta**. Hii ni katika kutafsiri **maono** na kutekeleza **maelekezo** ya **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** katika **kuwatumikia Watanzania na kufikia matarajio yake na ya Serikali nayoiongoza, na kuwaachia tabasamu**.

Naomba **niwashukuru tena Wanahabari wote mliopo hapa kutoka vyombo mbalimbali vya habari (magazeti, radio, televisheni na mitandao ya kijamii) na wengine popote walipo, kwa ushirikiano mzuri mliotupatia na mnaoendelea kutupatia**, na **kwa kuufikishia umma habari mbalimbali zikiwemo za LATRA na huduma za udhibiti wa usafiri ardhini bila kuchoka**.

Mwisho, kwa wadau wetu na Watanzania wote kwa ujumla, tunawaomba tuendeleze **umoja, mshikamano, amani, upendo, utulivu, ushirikiano, kusaidiana na kuheshimiana** na kamwe **tusibaguane kwa rangi, dini, kabila, jinsia, kanda au rika.** Tuzidi kumuomba Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema na umri mrefu **Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, ili aendelee kutuongoza na kuijenga **Tanzania tunayoitaka kuelekea Dira 2050.**

***Asanteni sana kwa kunisikiliza.***

*Pamoja Kwa Usafiri Bora*



*CPA. Dkt.* Habibu J. S. Suluo

**MKURUGENZI MKUU**

## TAFSIRI ISIYO RASMI-YA AMRI YA WAZIRI WA FEDHA

**AMRI YA MIAMALA YA KIELEKTRONIKI (MALIPO YA LAZIMA KWA NJIA ZA KIELEKTRONIKI KWA MIAMALA ILIYOAINISHWA), 2026**

**TANGAZO LA SERIKALI NA. 158C**
**Limetangazwa tarehe 30/06/2026**

**SHERIA YA MIAMALA YA KIELEKTRONIKI, (SURA YA 442)**

AMRI

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 13(2))*

**AMRI YA MIAMALA YA KIELEKTRONIKI (MALIPO YA LAZIMA KWA NJIA ZA KIELEKTRONIKI KWA MIAMALA ILIYOAINISHWA), 2026**

**Jina na kuanza kutumika**

1. Amri hii itaitwa **Amri ya Miamala ya Kielektroniki (Malipo ya Lazima kwa Njia za Kielektroniki kwa Miamala Iliyoainishwa), 2026**, na itaanza kutumika tarehe **1 Julai 2026**.

**Malipo ya lazima kwa njia za kielektroniki**

2.-(1) Mtu anayefanya au kupokea malipo kuhusiana na muamala ulioainishwa katika Jedwali atalazimika kufanya au kupokea malipo hayo kupitia **njia ya kielektroniki**.

(2) Kwa madhumuni ya Amri hii, **"njia ya kielektroniki"** maana yake ni njia, mfumo au chaneli ya kufanya au kupokea malipo kwa kutumia teknolojia ya kielektroniki au kidijitali, ikijumuisha:

- fedha kwa njia ya simu (mobile money);
- uhamisho wa fedha kupitia benki;
- uhamisho wa fedha kielektroniki;
- kadi ya malipo;
- pochi ya kielektroniki (electronic wallet);
- kifaa cha mauzo na malipo (Point of Sale – POS);
- huduma za benki kupitia intaneti au simu; au
- mfumo wa Serikali wa malipo ya kielektroniki.

Masharti ya mpito

3.-(1) Mtu ambaye, mara moja kabla ya kuanza kutumika kwa Amri hii, alikuwa akipokea malipo kuhusiana na muamala ulioainishwa, atapaswa, ndani ya **miezi sita**, kuweka mfumo wa malipo ya kielektroniki kwa mujibu wa Amri hii.

(2) Amri hii haitaathiri mipango au mikataba kuhusu muamala wowote uliofanyika kabla ya Amri hii kuanza kutumika.

JEDWALI

**MIAMALA INAYOPASWA KUFANYWA KUPITIA NJIA ZA MALIPO YA KIELEKTRONIKI**

| Na. | Muamala |
|---|---|
| 1 | Malipo ya ada, tozo, ushuru, malipo ya matumizi ya barabara au nauli zinazohusiana na huduma za **mabasi yaendayo haraka (BRT), vivuko, madaraja, mabasi ya abiria ya masafa marefu, teksi mtandao, usafiri wa anga, usafiri wa reli na huduma za maegesho**. |
| 2 | Malipo ya bidhaa au huduma katika **maduka makubwa (shopping malls), kumbi za mazoezi, kumbi za sinema, vituo vya kujaza mafuta, kumbi za mikutano na matukio, viwanja vya michezo na maonesho ya biashara ya kimataifa**, kama vile Saba Saba na Nane Nane. |
| 3 | Malipo ya ada na michango kwa ajili ya huduma za elimu katika **shule za awali, msingi na sekondari, taasisi za elimu ya juu na vyuo vikuu**. |
| 4 | Malipo ya michango kwa ajili ya huduma za elimu katika **taasisi za elimu ya juu na vyuo vikuu**. |
| 5 | Malipo ya **malazi, chakula na vinywaji** katika hoteli, migahawa na mikahawa. |
| 6 | Malipo yanayohusiana na **huduma za utalii**. |
| 7 | Malipo yanayohusiana na **kukodisha, kuuza au kununua jengo, kiwanja au shamba**. |
| 8 | Malipo ya **kuuza au kununua magari**. |
| 9 | Malipo yanayohusiana na shughuli za kilimo zinazofanywa kupitia **vyama vya ushirika na Vyama vya Ushirika vya Masoko ya Mazao (AMCOS)** kwa mazao ya kimkakati, yakiwemo **pamba, korosho, kahawa, chai, mkonge na tumbaku**, pamoja na pembejeo za kilimo na viuatilifu. |

**Dodoma, 30 Juni 2026**
**KHAMIS MUSSA OMAR**
**WAZIRI WA FEDHA**